


JE UNAJUA UMUHIMU WA KUPANDA MITI NA FAIDA ZA MISITU?



Kwa nini tunahitajika kupanda miti?

Tupande miti kwani maisha yetu yanategemea sana miti. Miti ni uhai. Tunatakiwa kupanda miti na kuitunza ili ituletee faida.

Tupande miti ili tuokoe misitu yetu ya asili.

Je unaweza kupanda miti ya aina gani?

Ni vema upande miti ukiwa na malengo. Miti ipo ya aina nyingi. Aina mbalimbali za miti zina manufaa mbalimbali pia.

- Miti ya matunda / chakula: miembe, miparachichi, mikoroshu, michungwa, mifenesi na michenza.
- Miti ya mbao: mininga, mikongo, mivule, grevilea, mikangazi, mipaini na mikaratuzi.
- Miti ya kuni / nishati: mijohoro, grevilea.
- Miti ya kurutubisha ardhi: grevilea, mikesya, milusina.
- Miti ya dawa: milonge, miarobaini.

- Miti ya chakula cha mifugo: milusina.
- Miti ya kuhifadhi maji: mikuyu, mikangazi.
- Miti mingi inazuia mmomonyoko wa udongo na miti pia huzuia upepo mkali.

Je unaweza kupata wapi mbegu na miche ya miti?

Mbegu zinaweza kupatikana kwa kuokota kutoka kandokando au chini ya miti. Pia mbegu za miti zinaweza kununuliwa. Pata ushauri kutoka kwa Afisa misitu aliye karibu na eneo lako. Miche ya miti inapatikana kama maotea au katika kitalu cha miti.

Mafunzo juu ya upandaji na usimamizi wa miti yanapatikana wapi?

Waone wataalamu wa misitu, kamati za maliasili na mazingira, klabu za mazingira, mashirika na taasisi za kutunza misitu na mazingira mfano.